## 5. Suala kuu la mshikamano wa kitaifa

### Kusikiliza na kuzungumza

### Methali

### Methali zinazohusu umoja na ushirikiano

Sikilizeni methali zinazohusu umoja na ushirikiano zikitumika.

1. Wanakijiji hao walikuwa na uhaba wa maji kwa muda mrefu. Kila mmoja alikuwa akizitumia mbinu zake kuyatafuta maji. Walikuwa wakichimba visima vidogovidogo katika mashamba yao. Visima hivyo viliwapa maji kidogo tu na kwa muda mfupi kisha kukauka. Baadaye, waliungana na kuongezeana maarifa. Walikata shauri kushirikiana na kuchimba kisima kikubwa. Kwa muda wa miezi miwili, kisima chenye kina kikubwa ajabu kilikuwa tayari na shida ya maji wakaizika katika kaburi la sahau. Hakika, umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.

2. Kila mkulima kijijini alizifanya shughuli za kilimo akiwa peke yake. Jambo hilo liliwaletea wakulima hao hasara. Waliamua kuungana na kuwa wakizinunua pembejeo pamoja kwa bei ya jumla. Aidha, waliamua kuungana ili kuzitafutia bidhaa zao soko. Kutokana na kushirikiana huko, walizipunguza gharama za pembejeo. Aidha, waliyakuza mazao yao kwa bei nafuu. Waligundua kuwa jifya moja haliinjiki chungu.

3. Kwa miaka mingi, haki za watoto zilikiukwa katika kijiji chetu. Mara kwa mara, mwanakijiji mmojammoja angejitokeza na kulalamika kuhusu hali hiyo. Angenyamazishwa mara moja na waliozikiuka haki za watoto. Hali hiyo iliendelea kwa miaka mingi.

Mzee mmoja aliwakumbusha wanakijiji waliozipinga dhuluma zile kuwa umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu. Aliwashauri waungane. Waliungana na kuanzisha harakati za kuzitetea haki za watoto kwa pamoja. Wapinzani wao walijaribu kuwanyamazisha lakini wakashindwa. Muda si muda, ukiukaji wa haki za watoto ulimalizika kijijini.

4. Eneo hilo la kijiji lilikuwa likikatwa miti ovyoovyo. Kijana aliyeitwa Pelo alijaribu kuwahamasisha wanakijiji kuithamini miti. Juhudi zake hazikuzaa matunda. Hatimaye, aliamua kuwashirikisha vijana wenzake katika juhudi zake. Pelo aliwaleta pamoja vijana na kuunda kikundi. Kikundi hicho cha vijana kilishirikiana

kuwahamasisha watu kuhusu kuitunza miti. Vijana hao walishirikiana kuzipanda mbegu za miti kisha kuwapa wanakijiji miche ili waipande. Vilevile, walishirikiana kuwapa mafunzo kuhusu namna ya kuitunza miti. Polepole, wanakijiji walianza kuithamini miti. Kumbe wahenga hawakukosea waliposema kuwa kinga na kinga ndipo moto huwaka!